

Maswali na Majibu (Mipira wa Kiume)

Q. Kwa nini utumie mipira?

A. Mpira waweza kuwalinda wewe na mpenzi wako kutokana na kuambukizana Virusi vya ukimwi na magonjwa yanayotokana na kufanya mapenzi au kushirikiana kimwili na mwenzako.

Q. Je, mipira ya kiume hufanya kazi?

A. Ndio, ingawapo zitatumiwa vizuri kabla ya wakati wake wa kuharibika.

Q. Je ninaweza nikatumia mipira miwili kwa mtu nisiyemfahamu ilikujikinga zaidi?

A. La, hii itasababisha mipira kuraruka.

Q. Naweza kuzungumza na mpenzi wangu kuhusu mipira ya kiume?

A. Unaweza ukatumia dalili kidogo wakati unaofaa. Dalili hizi zaweza kuwa rahisi kama kuwa na mipira karibu nawe.

Hata hivyo mazungumzo na mpenzi wako ndio njia bora kabisa. Hii yaweza ikakuwa jinsi ya kuanzisha mazungumzo kwa kusema : "Hufikiri kwamba siku hizi kila mtu ni lazima afanye mapenzi kama amejilinda ?" ama, kwa jumla waweza ukasema " Kama ningalikua nianze kufanya uhusiano wa kimapenzi ningalitumia mipira" ndivyo mpenzi wako awezo kujua msimamo wako. Wakati mwingine njia hizi zaweza kukosa mafanikio, Kwa hivyo kuna njia zingine zaweza kutumika kuwasisitiza wapenzi wetu kutumia mipira ni kama:

" Wajua yakwamba nahisi kuvaa mpira kukinifurahisha sana" ama "kutumia mipira hunifanya kupata raha zaidi na kuhisi nimetulia vyema."

Mipira husaidia kuzuia magonjwa yanayo tokana na kufanya mapenzi na virusi vya ukimwi ama pia kuzuia mimba kwani pia mipira ni njia ya kupanga uzazi – njia ya kipekee ya kupanga uzazi ambayo pia inazuia uambukizana wa virusi vya ukimwi.

Pia kuna njia mingi za kuanza mazungumzo kama kusema : " watu wale ambao wanatumia mipira ni lazima wawe wanaheshimiana na kupendana sana sababu wanahakikisha wato wamejikinga na wako salama " ama wewaza kusema " Nafikiri wanaume wale hutumia mipira wako bora kufanya mapenzi sababu wanauwezo wakakawia wakifanya mapenzi."

Q. Je mpenzi wangu akisema kuwa simwamini?

A. Jibu rahisi ni kumweleza " Wajua nakujali sana na mmoja kati yetu aweza akawa na virusi bila kuwa na fahamu kwamba anazo.

Q. Je mpenzi wangu akisema kuwa mipira haipendezi?

A. Mara mingi wanaume husema kwamba mipira hupunguza raha ambayo wanahisi kwa hivyo hawataki kuzitumia. Kuzungumzia swala hili, tunaweza tukatumia njia ama jinsi zilizozungumziwa hapo awali za kutumia mazungumzo na mpenzi wako, kama " tunapendana lakini hatufahamu kama mmoja wetu ana virusi." Unaweza pia ukasema " basi wacha tujaribu mara kadhaa ndivyo tuwache kuwa na wasiwasi." Kama mpenzi wako anazidi kukataa, waweza ukasema kuwa umeskia wanaume hukawia sana wakifanya mapenzi wakati wanapotumia mipira na pia hufanya kufanya mapenzi iwe bora zaidi. Mwishowe mtu aweza kukataa kufanya mapenzi bila mipira.

Kuna pia mipira ya kiume mpya iliyotengenezwa kuongeza raha zaidi, hii yaweza kukabiliana na fikra kwamba mipira haipendezi.

`Pronto Condoms` kama mipira hii mpya inavyojulikana inasemekana kuweza kuvaliwa kwa sekunde moja.